**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UCHUKUZI**

**MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI**

# TAARIFA KWA UMMA

## AMRI YA BODI YA WAKURUGENZI KUHUSU MAREJEO YA NAULI ZA MABASI YA MASAFA MAREFU NA MIJINI (DALADALA)

### 1.0 UTANGULIZI

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) ilipokea maombi kutoka kwa makampuniya utoaji huduma ya usafiri wa abiria ya Super Feo Enterprises, ABC Classic na HappyNation wakiiomba Mamlaka kufanya marejeo ya nauli za mabasi kufuatia ongezeko lagharama za uendeshaji, ikiwemo kupanda kwa bei ya mafuta (petroli na diseli). Mapendekezo ya makampuni haya ni kuongeza **nauli ya sasa ya Shilingi 56.88 kwakilometa** kwa abiria kama ifuatavyo:

| Na. | Kampuni | Aina ya Huduma | Nauli Pendekezwa kwa Kilometa | Ongezeko | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Shilingi | Shilingi | % |
| 1. | Super Feo Enterprises | Daraja la Kati | 101.88 | 45.00 | 79.11 |
| 2. | ABC Upper Class and Transportation Ltd | Daraja la Kati | 92.84 | 36.96 | 63.22 |
| 3. | Happy Nation Co. Ltd | Daraja la Kati | 84.06 | 27.18 | 47.78 |

Kwa kuzingatia kifungu cha 21 cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini, Suraya 413 pamoja na kanuni ya 9(3) ya Kanuni za Tazo za Mwaka 2020 (Tangazo la Serikali Na. 82 la tarehe 7/2/2020), Mamlaka iliitisha Mkutano wa Wadau uliofanyika **Dar es Salaam, Jumatano, tarehe 18 Oktoba, 2023, katika ukumbi wa Arnaoutouglou**, ili kutoa fursa kwa makampuni haya kuwasilisha mapendekezo yaokwa wadau na kisha kukusanya maoni ya wadau. Aidha, kwa kuzingatia kanuni ya 13ya Kanuni za Tozo, LATRA ilitumia Mkutano huo kuwasilisha mapendekezo ya marejeo ya nauli za mabasi ya mijini (daladala). Vilevile, taarifa za wadau wengine zilizopokelewa (Said & Brothers na DARCOBOA) zilitumika katika uchambuzi.

## 2.0 UTARATIBU WA KUFANYA MAREJEO YA NAULI

### 2.1 Mtoa Huduma Kuwasilisha Maombi au LATRA Kuanzisha Mchakato

Kanuni ya 9(2) ya Kanuni za LATRA (Tozo) za Mwaka 2020 (Tangazo la Serikali. Na. 82 la tarehe 7/2/2020), inaelekeza kwamba mtoa huduma anaweza kuwasilisha maombi ya kufanya marejeo ya tozo (nauli) baada ya angalau miaka mitatu (3) tangumarejeo ya mwisho kufanyika. Kwa nauli hizi za mabasi, marejeo ya mwisho yafanyikana kuanza kutumika tarehe 6 Mei, 2022. Hivyo, haikufika miaka mitatu.

Hata hivyo, kanuni ya 9(3) ya Kanuni za LATRA (Tozo) za Mwaka 2020 (Tangazo la Serikali. Na. 82 la tarehe 7/2/2020), inaelekeza kuwa, bila kujali kanuni ya 9(2), endapo rejesho la mtaji (*return on investment*) ya mtoa huduma itakuwa chini ya asilimia 10, anaweza kuwasilisha maombi kwa LATRA ndani ya mwaka mmoja ya kufanyiwa marejeo ya nauli. Mawasilisho ya watoa huduma yalionesha rejesho la mtajikuwa chini ya asilimia 10. Kanuni ya 9 (4) inaruhusu mtoa huduma kuwasilisha maombi kwa niaba ya watoa huduma wengine wanaotoa huduma zinazofanana.

### 2.2 Fomu ya Maombi na Nyaraka Zinazohitajika

Kwa mujibu wa Kanuni ya 9 (1) ya Kanuni za LATRA (Tozo) za Mwaka 2020 mtoa huduma anatakiwa kuwasilisha maombi ya marejeo ya nauli kwa kujaza fomu maalumu inayopatikana kwenye Jedwali la Pili pamoja na kuambatisha nyaraka zifuatazo:

(i) Leseni hai ya LATRA;
(ii) Nauli inayopendekezwa;
(iii) Sababu na hoja ya kupendekeza marejeo na pamoja na faida kwa watumiaji(abiria) kwa kufanya marejeo hayo;
(iv) Kikokotoo kilichotumika kufikia kwenye mapendekezo ya nauli;
(v) Hesabu zilizokaguliwa kwa miaka mitatu mfululizo iliyopita, au pungufu ya miaka mitatu kulingana na umri wa kampuni;
(vi) Taarifa ya Utendaji wa Kampuni kwa miaka mitano iliyopita au pungufu kutegemeana na umri wa kampuni; na
(vii) Taarifa nyingine yeyote ya ziada itakayotakiwa na LATRA.

### 2.3 LATRA Kufanya Mchakato wa Marejea Bila Maombi

Kanuni ya 13(1) ya Kanuni za LATRA (Tozo) za Mwaka 2020 (Tangazo la Serikali Na. 82 la tarehe 7/2/2020), inairuhusu LATRA kufanya marejeo ya nauli hata kama haijaletewa maombi, kwa kuzingatia kutokea kwa mambo yafuatayo:

i) Mabadiliko katika mazingira yanayosababisha kufanya marejeo ya nauli;
ii) tozo (nauli) zinazotozwa na mtoa huduma hazikuwa zimeidhinishwa na LATRA;
iii) viashiria na mapendekezo yaliyotumika kupanga tozo (nauli) zilizopo zimebadilika sana; au
iv) mtoa huduma ameshindwa kuwasilisha maombi LATRA kwa wakati.

## 3.0 UCHAMBUZI WA MAOMBI YA WATOA HUDUMA NA MAONI YA WADAU

Uchambuzi wa maombi ya watoa huduma pamoja na maoni ya wadau yaliyowasilishwa kwa maandishi na yaliyotolewa kwenye Mkutano wa Wadau,ulifanyiwa uchambuzi na Jopo lililojumuisha Wataalamu wa Fedha, Uchumi, Sheria,Takwimu na Usafiri na Usafirishaji. Uchambuzi wa Jopo la Wataalamu namapendekezo yao yaliwasilishwa kwenye ngazi ya Menejimenti ya LATRA kwamarejeo, na kisha Menejimenti iliwasilisha mapendekezo yake kwa Bodi yaWakurugenzi kwa maamuzi.

Uchambuzi umeonesha kwamba sababu za kufanya marejeo ya nauli sio kupanda kwa bei za mafuta pekee. Sababu zingine zilizozingatiwa na zipo kwenye kikokotoo cha Mdhibiti (LATRA) ni gharama za uwekezaji (capital cost) na za uendeshajizikijumuisha (operating costs) ikiwa ni gharama za matengenezo ya gari, kubadilishamatairi, bima, kodi ya mapato, tozo za Halmashauri, ada na tozo za LATRA, uchakavu (depreciation), ukaguzi wa magari, mishahara ya madereva na makondakta. Masualamengine yaliyozingatiwa ni uwezo wa gari (idadi ya abiria), ujazo (occupancy ratio), muda wa matumizi ya gari na tairi zake, idadi ya siku za matumizi ya gari kwa mwaka, wastani wa idadi ya safari na idadi ya abiria watakaosafirishwa. Aidha, uchambuzi ulizingatia uwezekano wa kuendelea kupanda kwa bei nishati ya mafuta.

Bodi ya Wakurugenzi ya LATRA, katika kikao chake cha kawaida cha 12 kilichofanyikatarehe 25 Oktoba, 2023 ilipokea, kuchambua na kufanyia maamuzi mapendekezo yaMenejimenti kuhusu marejeo ya viwango vya nauli za mabasi ya masafa marefu na mijini (daladala). Bodi ilijiridhisha kwamba nauli zilizorejewa zimezingatia mambo ya

msingi yatakayofanya huduma iendelee kupatikana na watumiaji wa huduma waendelee kumudu nauli hizo na kupata huduma ya usafiri. Aidha, Bodi iliridhika kwamba ukokotoaji huo wa nauli ulitumia kiwango cha rejesho la mtaji (*return on investment*) la asilimia 12 kama baadhi ya watoa huduma walivyoomba ili waweze kutoa huduma ya usafiri ulio ubora na kwa ufanisi.

Maamuzi ya Bodi kwenye kurejea viwango vya nauli ya mabasi yalikuwa kama inavyooneshwa kwenye Jedwali la Kwanza (Nauli za Mabasi ya Mijini (Daladala) na Jedwali la Pili: Nauli za Mabasi ya Masafa Marefu hapa chini:

**Jedwali la Kwanza: Mabasi ya Mijini (Daladala)**

| Umbali wa Ruti | Nauli ya Sasa (Sh) | Nauli Iliyo-chakatwa (Sh) | Nauli pende-kezwa (Sh) | Ongezeko | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Sh | % |
| Usiozidi Kilomita 10 | 500 | 601.22 | 600 | 100 | 20.0 |
| Kuanzia Kilomita 11 hadi 15 | 550 | 685.14 | 700 | 150 | 27.3 |
| Kuanzia Kilomita 16 hadi 20 | 600 | 804.08 | 800 | 200 | 33.3 |
| Kuanzia Kilomita 21 hadi 25 | 700 | 897.22 | 900 | 200 | 28.6 |
| Kuanzia Kilomita 26 hadi 30 | 850 | 1,087.64 | 1,100 | 250 | 29.4 |
| Kuanzia Kilomita 31 hadi 35 | 1,000 | 1,284.87 | 1,300 | 300 | 30.0 |
| Kuanzia Kilomita 36 hadi 40 | 1,100 | 1,407.66 | 1,400 | 300 | 27.3 |

**Jedwali la Pili: Mabasi ya Masafa Marefu**

| Daraja | Hali ya Barabara | Nauli ya Sasa (Sh.) | Nauli Mpya (Sh.) | Ongezeko | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Sh. kwa Km | Asilimia |
| **Kawaida (Ordinary Bus)** | Lami | 41.29 | 48.47 | 7.18 | 17.39 |
| | Vumbi | 51.61 | 53.32 | 1.71 | 3.31 |
| **Kati [Semi Luxury Bus (Upper & Lower)]** | Lami | 56.88 | 67.84 | 10.96 | 19.27 |

**Tanbihi:** Nauli hizi zinajumuisha tozo ya LATRA ya asilimia 0.5 (0.005) ya nauli.

## 4.0 AMRI YA BODI YA WAKURUGENZI

Katika hatua ya kuzingatia utawala bora, Mamlaka iliwasilisha Wizara ya UchukuziTaarifa ya maamuzi ya Bodi ya Wakurugenzi ya marejeo ya nauli hizi kabla ya kutoa

Amri ya Bodi kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali kwa kuzingatia Sheria. Hivyo, baada ya kuridhiwa na mamlaka husika, Amri ya Bodi ilitangazwa kwenye Gazeti la Serikali, Taarifa ya Kawaida Na. 6935, Toleo Na. 47 ya tarehe 24 Novemba, 2023. Taarifa hiyo inasomeka kama ifuatavyo:

**MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI**

**TAARIFA KWA UMMA**

**AMRI YA BODI**

*(Imetolewa chini ya kifungu cha 19 cha Sheria ya LATRA, Sura ya 413)*

**MAREJEO YA NAULI ZA USAFIRI WA MABASI YA MASAFA MAREFU NA MIJINI**

Kifungu cha 19 cha Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini, Sura ya 413 imeipa Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini (LATRA) jukumu la kupanga na kufanyamarejeo ya tozo za huduma ya usafiri ikiwa ni pamoja na nauli za mabasi.

Mamlaka inautangazia umma kuhusu marejeo ya nauli za mabasi ya masafa marefu na mijini (daladala) kama zinavyoonekana kwenye Jedwali la Kwanza na Jedwali la Pili hapa chini, mtawalia:

**JEDWALI LA KWANZA**
**NAULI ZA MABASI YA MASAFA MAREFU**

**Nauli za Mabasi ya Masafa Marefu kwa Abiria kwa Kilometa**

| Daraja la Basi | Hali ya Barabara | Nauli iliyoidhinishwa |
|---|---|---:|
| Kawaida (Ordinary Bus) | Lami | 48.47 |
| | Vumbi | 53.32 |
| Kati (Semi Luxury Bus) | Lami | 67.84 |
| | Vumbi | - |

**JEDWALI LA PILI**

**NAULI ZA MABASI YA MIJINI (DALADALA)**

| Na. | Umbali wa Njia | Nauli (SH.) |
|---|---|---|
| 1 | Usiozidi Kilomita 10 | 600 |
| 2 | Kuanzia Kilomita 11 hadi 15 | 700 |
| 3 | Kuanzia Kilomita 16 hadi 20 | 800 |
| 4 | Kuanzia Kilomita 21 hadi 25 | 900 |
| 5 | Kuanzia Kilomita 26 hadi 30 | 1,100 |
| 6 | Kuanzia Kilomita 31 hadi 35 | 1,300 |
| 7 | Kuanzia Kilomita 36 hadi 40 | 1,400 |

## Nauli ya Mwanafunzi

Nauli ya mwanafunzi kwa mabasi ya mijini (daladala) kwa umbali wa njia zoteitaendelea kuwa **shilingi 200 kwa kila safari**.

## MAMBO YATAKAYOFUATILIWA NA LATRA

LATRA inawaelekeza watoa huduma wa usafiri wa mabasi ya masafa marefu na mijini (daladala) kuzingatia yafuatayo:

### (a) Mabasi ya Masafa Marefu

(i) Nauli zinazotozwa zisizidi ambazo zimetolewa kwenye Tangazo hili.

(ii) Madereva na wahudumu (makondakta) kuvaa sare safi na nadhifu.

(iii) Mtoa huduma kutotoza nauli zaidi ya umbali anaoenda abiria.

(iv) Basi liwe safi wakati wote na kupuliza dawa ya kuua wadudu.

(v) Kutumia mfumo unaoruhusu abiria kuchagua kiti na kukata tiketi mtandao.

(vi) Kuweka alama kwenye mizigo (luggage tags) kuepuka upotevu.

(vii) Kuwatumia madereva waliothibitishwa na LATRA.

(viii) Kuhakikisha matumizi ya kitufe cha utambuzi wa dereva (*i-button*).

(ix) Kutokuweka miziki na/au nyimbo na picha (video) zilizo kinyume na maadili ya Kitanzania.

(x) Kuzuia mahubiri ya aina yoyote na kuzuia kufanya biashara ndani ya basi.

(xi) Kutunza mazingira kwa kuweka chombo cha kuhifadhi uchafu ndani ya basi.

(xii) Kusimama sehemu zenye huduma za kijamii kwa angalau dakika 20.

**(b) Mabasi ya Mijini (Daladala)**

(i) Nauli zinazotozwa zisizidi ambazo zimetolewa kwenye Tangazo hili.

(ii) Madereva na wahudumu (makondakta) kuvaa sare safi na nadhifu.

(iii) Mtoa huduma kutotoza nauli zaidi ya umbali anaoenda abiria.

(iv) Basi liwe safi wakati wote na kupuliza dawa ya kuua wadudu.

(v) Nauli ziandikwe ubavuni mwa gari upande wa mlango wa kuingia abiria.

(vi) Kutokatisha njia (route) ya safari.

(vii) Kutokuweka miziki na/au nyimbo na picha (video) zilizo kinyume na maadili ya Kitanzania.

(viii) Kuzuia mahubiri ya aina yoyote na kuzuia kufanya biashara ndani ya basi.

Hivyo, Mamlaka inatoa Notisi ya siku 14 kuanzia tarehe ya kutangazwa kwa taarifa hii,kwamba yeyote ambaye hataridhishwa na Amri hii anaweza kukata rufaa Baraza la Ushindani. Baada ya kumalizika siku 14, endapo hakutakuwa na rufaa yoyote, nauli hizi zitaanza kutumika rasmi.

Imetolewa leo tarehe **20** Mwezi **Novemba** Mwaka **2023.**

AHMED MOHAMED AME
**MWENYEKITI WA BODI**
**MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI**
**MAKAO MAKUU - DODOMA**

## 5.0 HITIMISHO

Amri ya Bodi itaanza kutekelezwa rasmi tarehe 8 Desemba, 2023 endapo hakutakuwa na pingamizi yeyote. Menejimenti imeandaa Jedwali za Nauli kwa ajili ya uelewa wa mabadiliko yaliyo katika Amri hii (Rejea Kiambatisho Na. 1). Nauli za Njia za Mikoa yote itatangazwa kwenye tovuti ya LATRA (www.latra.go.tz).



Digitally Signed By Habibu J. S. Suluo
Mon Nov 27 12:54:13 EAT 2023

Habibu J. S. Suluo

**MKURUGENZI MKUU**